

# HALMASHAURI YA WILAYA YA IGUNGA

SHULE YA SEKONDARI MBUTU,  
S.L.P 207,  
IGUNGA.  
08/12/2020.

Kumb.Na. MBSS/EL/K1/12  
MZAZI/MLEZI WA .....  
SHULE YA MSINGI.....  
IGUNGA.

## YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA ELIMU YA SEKONDARI KIDATO CHA KWANZA SHULE YA SEKONDARI MBUTU-2021

Nafurahi kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na elimu ya sekondari kidato cha kwanza katika shule yetu mwaka 2021. Shule ipo Km 10 toka makao makuu ya wilaya Igunga, Mkoa wa Tabora. Masomo katika muhula wa kwanza yataanza tarehe 11/01/2021. Unapaswa kuletwa shuleni na mzazi/mlezi ili kusajiliwa siku hiyo kuanzia saa 1:00 asubuhi.

Unahimizwa kumshonea mwanao sare za shule na michezo kwa idadi kama ifuatavyo:

### (a) Sare za shule:-

1. Wavulana suruali 2- Damu ya mzee, mashati meupe 2 aina ya tetroni mikono mifupi
2. Wasichana sketi 2- Damu ya mzee, mashati meupe 2 aina ya tetroni mikono mifupi
3. Wavulana na wasichana-viatu vyeusi vya ngozi visigino vifupi jozi 2, soksi nyeupe jozi 2

NB: SKeti ziwe za kitambaa zenye marinda makubwa ndefu chini ya magoti, suruali kwa wavulana zenye marinda (celebration) na mkanda mweusi wa kuvaliwa kiunoni.

(b) Wavulana na wasichana –Tai ndefu rangi ya damu ya mzee

(c) Wavulana waishio nje ya kijiji cha mbutu waje na magodoro madogo saizi 3x6 wataishi Hostel, shuka 2 light blue, ndoo ndogo 1 ya maji ,mto 1

(d) Sweta 1 rangi ya damu ya mzee-ili kujikinga na baridi

### (e) Sare za michezo

(i) Wavulana –Bukta 1 nyeusi, fulana 1 blue

(ii) Wasichana –Bukta 1 nyekundu, fulana 1 blue

-Raba jozi 1 nyekundu/ six meno na soksi ndefu hadi magotini

### (f) Vifaa vya darasani

- Daftari 10 aina ya counter book quire 3, kalamu ya wino blue/black, Mkebe 1 wa Hisabati.

### (g) Maagizo kwa Mzazi

i. Shule yetu inatoa chakula cha mchana kwa wanafunzi wa kutwa na pia chakula cha mchana na usiku kwa wanafunzi a Hostel. **CHAKULA HUSIMAMIA NA KAMATI YA WAZAZI**; Ili kujua mahitaji ya chakula piga simu kwa mjumbe wa kamati ya chakula, **MZEE LUHENDE** kwa namba **0785315486**

ii. Apimwe afya na kuleta Medical Examination Report

iii. Mwanafunzi na Mzazi/Mlezi watajaza mkataba kufuata sheria za shule na maagizo ya serikali yatakayotolewa

iv. Kama mwanafunzi hataletwa shuleni zaidi ya wiki moja (1) baada ya shule kufunguliwa mzazi atashitakiwa MAHAKAMANI.

**Mzazi: Kumbuka kula chakula kwa mtoto mchana akiwa shuleni inaweza saidia kuboresha maendeleo ya ufaulu mzuri kwa mtoto wako na kwa shule yetu kwa ujumla.**

**KARIBUNI MBUTU SEKONDARI**

  
**ABAS MOHAMED ANDIKA**  
MKUU WA SHULE

**MKUU WA SHULE**  
**SHULE YA SEKONDARI MBUTU**  
**IGUNGA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA IGUNGA  
SHULE YA SEKONDARI MBUTU**

(Uende na fomu hii kwa Mganga wa Hospitali ya Serikali kwa ajili ya vipimo)

MGANGA/DAKTARI

HOSPITALI YA.....

S.L.P .....

**MEDICAL CERTIFICATE**

Jina la Mwanafunzi.....kidato.....umri.....

Afya yake kwa ujumla

(a) Kifua .....

(b) Masikio .....

(c) Macho .....

(d) Akili .....

(e) Kilema chochote kitaje.....

(f) Mkojo.....

(g) Choo(stool).....

1. Kwa wasichana tu.Nimemwona anamimba/hana  
mimba.....

Mengineyo .....

2. Nimempima mtajwa hapo juu na nimemwona amepatikana na  
ugonjwa.....

3. Nimempima mtajwa hapo juu na nimemona anaweza/hawezi kusoma kwa  
sababu.....

.....  
.....

.....  
**JINA NA SAHIHI YA MGANGA**

.....  
**CHEO**